

MAOMBI KWA DAMU YA YESU

Imba nyimbo hii kabla ya kuomba maombi haya.

Damu ya Yesu (×3) Husafisha kabisa.

Nguvu za Shetani zimeshindwa (×3) Asifiwe Mwokozi!

Nguvu za mizimu zimeshindwa (×3) Asifiwe Mwokozi!

Nguvu za magonjwa zimeshindwa (×3) Asifiwe Mwokozi!

Sisi tunaimba Haleluya (×3) Asifiwe Mwokozi!

Siku moja Yesu atarudi! (×3) Asifiwe Mwokozi!

Yesu, wewe ni Mungu. Ninasema asante kwa ukombozi wako kupita damu yako. Ninaipenda sana damu yako iliyomwagika pale msalabani kwa ajili ya dhambi zangu. Wewe ulisema katika Mathayo 26:28 “kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi”.

Yesu, asante kwa kuninunua kwa damu yako ya thamani. Ninakiri mimi ni wako ulieninunua kwa damu yako mwenyewe kama neno lako linavyosema katika Matendo ya mitume 20:28 kuwa kanisa lako umelinunua kwa damu yako mwenyewe.

Mimi ni wa Yesu tena nimenunuliwa kwa damu yake mwenyewe . Mimi sio wako shetani, mimi sio wenu mizimu, mimi sio wenu mapepo, mimi sio wenu wachawi, mimi sio wenu waganga, mimi sio wenu laana, mimi sio wenu magonjwa, mimi sio wenu tabu, shida. Mimi ni wa Yesu tena ameninunua kwa damu yake yeye mwenyewe sio damu ya mnyama, wala mwanadamu bali ni yake mwenyewe tena isiyo na dhambi , uchafu bali ni safi tena ni takatifu na yenye nguvu.

Najitoa kwenye maagano nilioingia kwa damu ya mnyama, ya mtu, kwa kitu chochote kile. Mimi ni wa agano jipya la damu ya Yesu. Iliyo mwagika pale msalabani kama ilivyo andikwa katika Yohana 19:34 “lakini askari mmojawapo alimchoma ubavu kwa mkuki; na mara ikatoka damu na maji”. Leo ninajiondoa kwenye maagano hayo yote. Niliyofanya na mwanamke au mwanaume, na yoyote yanayo kwenda kinyume cha maisha yangu na mpango wa Mungu. Nina ya vunja sasa kwa damu ya agano jipya la Yesu Kristo. Kila agano nilofanya kwa kujua au kwa kutokujua, iwe mchana au usiku, nikiwa kwenye ndoto au macho, kwa hiali au kwa kulazimishwa ninayavunja sasa maagano hayo kwa damu ya Yesu Kristo wa Nazareth. Ninatangaza sasa katika ulimwengu wa roho na wa kawaida mimi ni wa Yesu sio wa shetani, mizimu, mapepo, majini, laana, magonjwa mimi ni wa Yesu.

Ninaliamini agano lako Yesu kwa damu yako. Hata Mathayo 26:28 umesema “kwa maana hii ndiyo damu yangu ya agano, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi”.

Kwenye damu kuna uhai (kumbukumbu la torati 12:23). Ukasema katika Yohana 6:53-56 “ amin, amin, nawaambieni, Msipoula mwili wake Mwana wa Adamu na kuinywa damu yake, hamna uzima ndani yenu. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu anao uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho. Kwa maana mwili wangu ni chakula cha kweli, na damu yangu ni kinywaji cha kweli. Aulaye mwili wangu na kuinywa damu yangu hukaa ndani yangu, nami hukaa ndani yake” Bwana nina amini maneno hayo. Nami ninafanya tendo la imani kwa kuinywa damu yako sasa.(Fanya kama unakunywa damu kwaimani)

Na kunywa damu ya Yesu ×10

Kila chakula nilichokula katika meza ya maadui, ya mapepo, mizimu, makaburini, baharini, ziwani, mtoni, sehemu yoyote ile. Kama ilikuwa mchana au usiku, kama ilikuwa kwenye ndoto au nikiwa macho, kwa kujua au kutokujua, kwa hiali au kwa kulazimishwa iwe ni chakula au vinywaji, sasa ni na viamuru kwa damu ya Yesu Kristo wa Nazareth vitoke ndani ya tumbo langu. Ni vitapike sasa kwa damu ya Yesu.

Tumbo langu kwa ajili ya mwili wa Yesu na damu yake sio vyakula na vinywaji vya kishetani au mizimu au mapepo. Nina vitapika sasa kwa damu ya Yesu. Nakuamuru sasa toka ndani yangu huna chako sasa. Kama umejificha sehemu yoyote natuma damu ya Yesu hapo. Toka sasa hapo ulipo iwe ni kwenye kitovu, kwenye tumbo, kwenye ulimi, kwenye kiganja, kwenye kucha, kwenye shingo kwenye uso au kwenye nyayo za miguu. Ninakuamuru sasa kwa damu ya Yesu Kristo iliyo mwagika pale msalabani toka sasa achia hiyo sehemu. Siyo yako kwa Jina la Yesu Kristo wa Nazareth.

Nina kikomboa kitovu changu kutoka kwa mababu zangu, mabibi zangu, mizimu, mapepo, majini, maagano katika jina la Yesu Kristo wa Nazareth. Ninakifungua kila sehemu kilipo kuwa kimefungwa kwa damu ya Yesu. Nina tangaza kuwa kitovu changu kipo huru sasa kutoka kwenye maagano, mizimu, mashetani, mapepo, mababu, mabibi na kila eneo kilipo kuwa kimefungwa.

Ninakomboa damu yangu sasa kwa damu ya Yesu Kristo. Damu yangu iliyotumika katika maagano, matambiko ya kimila au kichawi, kiganga. Ninaikomboa sasa kwa damu ya Yesu. Kila kuchanjwa chale katika mwili wangu iwe na wazazi wangu, mabibi zangu, mababu zangu, wachawi au mapepo, mizimu, majini nakufuta sasa kwa damu ya Yesu. Nina safisha sasa mwili wangu na damu yangu kwa Damu ya Yesu Kristo. Kila silaha iliyokuwa imetumwa kwa kupandikizwa katika damu kwa chale ninaifuta sasa kwa damu ya Yesu. Kila silaha itakayofanyika juu yangu haitafanikiwa na kila ulimi utakaoinuka juu yangu katika hukumu utauhukumu kuwa mkosa (Isaya 54:17). Damu yangu imekombolewa sasa kwa damu ya Yesu. Kila udhaifu katika damu yangu, magonjwa, uchawi, uganga na uondoa kwa damu ya Yesu sasa. Ninakiri mimi nipo huru sasa.

Nina amini kuwa katika wewe, kwa damu yako, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema yako (Waefeso 1:7). Sisi tuliokuwa mbali hapo kwanza tumekuwa karibu kwa damu yako Kristo (Waefeso 2:13). Nafsi yako imekwisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wako (Wakolosai 1:20). Nina ujasiri wa kupaingia patakatifu kwa damu ya Yesu (Waebrania 10:19).

Waebrania 12:24 “ Yesu mjumbe wa agano jipya , na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili”. Yesu, damu yako inene mema katika maisha yangu, afya yangu, familia yangu, watoto wangu(majina), mume wangu, mke wangu, kazi yangu, na kila nikifanyacho damu yako inene mema juu yake. Na amini katika hiyo damu. Na ninaipenda sana damu hiyo.

Nimeshinda kwa damu yako. kama neno lako linavyosema katika ufunuo wa Yohana 12:11 kwamba Nao wakamshinda (joka, Ibilisi na Shetani {Ufunuo 12:9}) kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa. Na mimi nimeshinda kwa damu yako. Wala sio mkia tena mimi ni kichwa. Si wa shetani, mizimu, mapepo, maagano, mababu, mabibi, wachawi, waganga, majoka mimi ni wa Yesu Kristo wa Nazareth.

Yesu nashukuru kwa kumwaga damu yako kwa ajili ya maisha yangu, ndugu zangu, jamaa zangu. Kwa maana “Katika Torati karibu vitu vyote husafishwa kwa damu, na pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo”(Waebrania 9:22). Asante Yesu kwa jambo kubwa kama hili kwa ajili yangu. Nifunike kwa damu yako, funika mwili wangu, maisha yangu, familia yangu, afya yangu na kazi yangu. Nisaidie shetani asinishinde tena. Nakuamini ninakupenda katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareth. Amina.

By Innocent Morris

+255766259750

Instagram Page: **holyspiritconnect**